KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

THE QUR'AN & SUNNAH SOCIETY OF EAST AFRICA

AL-HUDAA [UONGOFU]

الهدى

25/= Ksh

Volume 24, Issue 1

16th Sha'baan 1433

6th JULY, 2012

KUWAKUFURISHA WAISLAMU BILA YA DALILI ZA KISHERIYA

NA: SHEIKH IBRAHEEM BIN 'AMIR AR-RUHAYLEE (حفظه الله)

YALIYOMO KATIKA JARIDA LA LEO

MWANZO WA UZUSHI WA ... 1 - 2

RIWAYA YA UZUSHI KATIKA ... 3 - 4

INGIA KWENYE UISLAMU KWA... 4

HABARI ZA MJI KWA MUKHTASAR

MASJID DHUN-NOORAYN WAFUNGULIWA RASMI:

Wakaazi wa Mtaa wa Kizingo wamebarikiwa katika siku za hivi karibuni kupata Miskiti mitatu mipya katika mtaa wao. Mbali na Masjid Ibraahim na Masjid Umm Kulthum, Sasa hivi Masjid Dhun-Noorayn katika uwanja wa mpira wa Congo Boys / Mwenge uko tayari kuanza kuswaliwa. Mskiti huo wenye takriban nafasi ya kiasi cha watu Mia Tano, utafunguliwa rasmi siku ya Ijumaa 23rd Sha'baan, 1433 tarehe sawiya na 13th July, 2012. Wakaazi wa mtaa huo watafurahia mno kwa kufunguliwa Mskiti huo utakaowawezesha kupata fursa ya ta'lim ya watoto wao na vilevile wanawake kuweza kuhudhuria vikao vya ki-Ilimu. Allaah Awahifadhi wasimamizi wa uwanja

Mwanzo wa kuwakufurisha watu pasi na dalili ulianza zamani katika historia ya Ummah huu, kiasi cha kwamba wanavyuoni wakataja yakwamba kuwakufurisha watu kutokana na madhambi ndiyo Bid'ah ya kwanza iliyojitokeza katika Ummah huu.

Amesema Sheikh ul Islam Ibn Taymiyyah: "Kwahivyo, hii ndiyo sababu ya kuwajibika kujitahadhari na kuwakufurisha Waislamu kutokana na madhambi yao na makosa yao. Kwa hakika ilikuwa ndiyo Bid'ah ya kwanza iliyojitokeza katika Uislamu. Kwahivyo, watu wake wakaanza kuwakufurisha Waislamu na wakahalalisha damu zao na mali zao [*Majmoo' fataawa 13/31, tizama katika "Sharh al-Asfahani Uk. 225*]. Watu wa kwanza walioanzisha kuwakufurisha watu kwa njia za kimakosa walikuwa ni ma-Khawaarij. Wao walikuwa ni wengi kwenye jeshi la 'Alee (رضي الله عنه) katika vita vya Siffeen, na pindi 'Alee na Mu'aawiya (رضي الله عنهم) walipokubaliana kusitisha vita baina yao, jambo lililotokea katika mwezi Mtukufu wa Ramadhaan kwenye mwaka wa 37 baada ya Hijra, hawa ma-Khawaarij walikataa azimio hilo. Walipinduka mipaka katika kumlaumu 'Alee mpaka wakamwambia: "Ulikuwa na watu waliostahiki kuhukumiwa na kitabu cha Allaah. Hapana Hukmu isipokuwa kwa [kitabu cha] Allaah," na wakamtangazia waziwazi ukafiri juu yake [Tizama katika *"al-Farq bayn al-Firaq"* cha al-Baghdadi Uk. 74-76; al-Bidaya wan Nihaya cha Ibn Katheer 10/577, na *Majmoo' fataawa* cha Sheikh ul-Islaam Ibn Taymiyyah 13/208].

Abul Hasan al-Ash'aree amesema: "Wameafikiana ma-Khawaarij katika kumkufurisha 'Alee Ibn Abee Twaalib (رضي الله عنه) kwa sababu alikuwa na watu waliohukumu kwenye mas'ala. Walikhitilafiana iwapo ukafiri wake ni Shirk au laa. Wameafikiana yakwamba kila dhambi kubwa ni ukafiri isipokuwa kwa an-Najdaat (kundi fulani la ma-Khawaarij) kwa vile wao hawatamki matamshi haya [makaalat al-Islaamiyyeen 1/167]. Baadhi ya wanavyuoni wametaja kwenye upekuzi wao kuhusu mapote yakwamba ma-Khawaarij wameafikiana kuwakufurisha: 'Alee, Uthmaan, na wale waliojitokeza kupigana kwenye vita vya Jamal, wale waliochukuwa hatamu za upatanishi, wale waliokubaliana na upatanishi, wale waliokubaliana na wapatanishi, au yakwamba mojawapo ya makundi lilikuwa sawa na kupingana na kiongozi dhalimu."

Kisha baada ya 'Alee (رضي الله عنه) kurudi kutoka kwenye vita vya Siffeen, ma-Khawaarij wakajitenga mahali peke yao paitwapo Haroora, ndipo walipojulikana kwa jina la Harooriyyah. Walikuwa ni watu 12,000. 'Alee (رضي الله عنه) akampeleka Ibn 'Abbaas (رضي الله عنه) ende akajadiliane nao. Nusu yao wakarudi nyuma na waliobaki wakaendelea na dhulma zao kwa kuwakosoa watu na kuzihalalisha damu zao. Ma-Khawaarij walimuuwa Abdullaah Bin Khubbab Bin al-Arrat, wakaingia ndani ya nyumba yake na kumuuwa mwanae wa kiume na mjakazi wake wa kike aliyekuwa mamake mwanae, na kisha wakakusanya jeshi lao wakiwa Nahrawaan. Kwahiyo, 'Alee (رضي الله عنه) akawaendea akiwa na jeshi lake la watu 4,000. Alipowakurubia, akamtuma mjumbe kutoka kwake akawaambie: "Watoeni waliomuuwa Abdullaah Bin Khubbab,"

(Endelea kwenye Uk. 2)

(Endelea Kutoka Uk. 1)

wakamrudisha mjumbe huyo kwa kumwambia aseme: “Sisi sote tumemuuwa Abdullaah Bin Khubbab”. ‘Alee (رضي الله عنه) akapigana nao, akawauwa wote isipokuwa watu tisa, na kwa upande wa ’Alee walikufa watu saba peke yake, na imesemekana yakwamba walikufa watu tisa.

‘Alee (رضي الله عنه) akaanza kutembea katika uwanja wa vita akiwatazama waliokufa miongoni mwa ma-Khawaarij, na huku akisema: “Nyinyi ni wadhalilifu kiasi gani, kwa hakika aliyewadanganya nyinyi ndiye aliyewadhuru.” marafiki zake wakamuuliza: “Ewe Ameer-il Mu’mineen, ni nani huyo aliyewadanganya?” Akawajibu, “Ni Shaytwan! Nafsi ya mwana-adamu imejiinamia kunako uovu, ikiwa inadanganywa na matamanio ya urongo na amewapambia madhambi. Tulidokezewa na Mtume yakwamba watatokea watu hao.” Kwa hakika, Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliwaambia Maswahaba zake kuwahusu ma-Khawaarij, yakwamba wata’asi na kwamba yeye alipendelea kupambana nao. Katika Swaheeh al-Bukhaari na Muslim kutoka kwenye hadeeth ya ‘Alee (رضي الله عنه) yakwamba alisema: “Nilimsikiya Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisema: ’Katika zama za mwisho, kutajitokeza vijana wadogo walio wapumbavu watakaosema maneno mazuri mno, lakini imani zao hazitozidi shingo zao na watatoka (wataiwacha) kwenye dini yao kama mkuki unavyoshopoka kutoka kwenye uta. Kwahiyo, popote mutakapowakuta, wauweni, kwani yoyote atakaewauwa atalipwa malipo mema Siku ya Kiyama.’” [Swaheeh *al-Bukhari* na *Fat-h* 12/283 (Hadeeth No. 6930) na *Muslim* 2/746 (Hadeeth No. 1066)].

AHAADEETH ZENYE KUWASHUTUMU MA-KHAWAARIJ

Amepokea al-Khallal kutoka kwa Imaam Ahmad (رحمه الله) yakwamba amesema: “ Ma-Khawaarij ni watu waovu mno, mimi sijawahi kuona watu waovu katika ardhi hii kama wao. Ahaadeeth zenye kuwahusu wao kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) ni swaheeh kutoka kwenye njia kumi.” [As-Sunnah cha Khalaal 1/145].

Sheykhul Islam Ibn Taymiyyah (رحمه الله) amesema kuhusu matamshi haya: “Imaam Muslim amezipokea kwenye kitabu chake as-Swaheeh na Bukhari amepokea baadhi yake.”

Kwahiyo, ma-Khawaarij ndiwo wa kwanza waliojulikana kwa kuwakufurisha Waislamu ki-makosa kutokana na madhambi. Lakini hatahivyo, hayo hayakukoma kwao peke yao, bali hata ma-Rawaafidh pia wanahusika kwenye kukufurisha huku kwa waliokuwa bora katika Ummah - Maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) - na wanaamini yakwamba Maswahaba walikufuru kwa sababu wali’asi utawala wa ’Alee (رضي الله عنه) kama wanavyodai wao.

Yaliyotajwa kwenye kitabu “al-Kaafi”, ambacho ndicho kitabu kilicho swaheeh mno miongoni mwa vitabu vyao kulingana na imani zao, imepokewa na Abu Ja’far - kama wanavyodai kuwa alisema: “Watu walikufuru baada ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), isipokuwa watu watatu.” Nikamuuliza, “Na ni watu gani hao watatu?”, akasema, “al-Miqdad Ibn al-Aswad, Abu Dharr al-Ghifaari na Salmaan al-Faarisy.”

Al-Mufeed, mmojawapo wa wanavyuoni wao wakubwa ametaja maafikiano ya Rawaafidh katika kuwakufurisha Maswahaba: “Imaamiyyah, Zaydiyyah na ma-Khawaarij wanaamini yakwamba makafiri na madhalimu miongoni mwa watu wa Basra na Shaam, wote ni makafiri, wapotofu na waliolaaniwa na kutokana na hayo, wao wako Motoni na watadumu humo milele.”

Ma-Rawaafidh ndiwo waovu zaidi miongoni mwa Ahlul-Bid’ah katika kukufurisha. Wao humkufurisha kila endae kinyume nao. Kwahivyo, wanaukufurisha Umma mzima kwa ujumla, wa Maswahaba na Taabi’een na wanavyuoni wote wa Dini hii na wala hawajiepushi na hayo kabisa.. Jambo hili ni maarufu kwao, kwa wenye kujua ’Aqeedah zao, na kusoma vitabu vyao.

Sheykhul Islam Ibn Taymiyyah (رحمه الله) amesema: “Ma-Rawaafidh walimkufurisha Abu Bakr, ‘Umar, ’Uthmaan na Muhaajireen na Answaar, na wale waliowafuata wao kwa wema, wale ambao Allaah aliokuwa radhi nao, nao wakawa radhi Nae. Ma-Rawaafidh waliwakufurisha watu wengi kwa ujumla katika Ummah wa Muhammad miongoni mwa waliotangulia na waliokuja baadae. Ma-Rawaafidh waliwakufurisha kila aliyeamini yakwamba Abu Bakr, ’Umar, Muhaajireen na Answaar walikuwa ni miongoni mwa watu wema au amewaridhia kama ambavyo Allaah alivyowaridhia, au mwenye kuwaombea Maghfirah (msamaha) kama ambavyo Allaah alivyoamrisha tuwaombee maghfirah. Kwahivyo, wao wamewakufurisha waheshimiwa katika Ummah huu, kama: Sa’eed Bin al-Musayyib, Abu Muslim al-Kholaani, Awais al-Qarni, ’Ataa’ Bin Abu Ribah, Ibraahim an-Nakha’ee, na mfano wa Maalik, Awza’ee, Abu Haneefah, Hamad Bin Zayd, Hamad Bin Salma, ath-Thawree, ash-Shaafi’ee, Ahmad Bin Hanbal, Fudhail Bin al-Ayyaad, Sulayman ad-Daraani, Ma’roof al-Karkhee, al-Junaid Bin Muhammad, Sahl Bin Abdullaah at-Tustaree, na wengineo vilevile. Ma-Rawaafidh wanaonelea yakwamba ukafiri wa Maswahaba ni mbaya zaidi hata kuliko ukafiri wa Mayahudi na Manaswara, kwa sababu ukafiri wao umechipuka kutoka kwenye mzizi, na hawa wengine walikuwa ni makafiri tu. Ukafiri wa kukufuru ni mbaya zaidi kama ilivyoafikiwa, hata pia kushinda Ukafiri wenyewe..” Kisha ugonjwa huu wa kuambukiza wa kuwakufurisha watu bila ya dalili ukahamia kutoka kwa ma-Khawaarij na ma-Rawaafidh hadi kwa Mu’tazilah. Bid’ah yao ilijitokeza kwenye mas’ala ya al-Qadar wakati wa mwisho wa zama za Maswahaba. Maswahaba walijiepusha kutokamana nao na Bid’ah zao. Sababu ya haya ilikuwa ni watu walikuwa wakijadiliana kuhusu hukmu ya mwenye kufanya madhambi makubwa, na haya yalikuwa ni baada ya ma-Khawaarij kuzua mfumo wa kuwakufurisha watu kutokana na kufanya madhambi. Ma-Qadariyyah nao walizungumza kuyahusu haya, nao wakakubaliana na ma-Khawaarij kwenye hukmu yao kuwahusu wenye kufanya madhambi ingawaje wakakhitilafiana kuhusu majina ya kuwapa.

Kuhusiana na haya Sheykhul Islam Ibn Taymiyyah (رحمه الله) amesema: “Kisha katika zama za mwisho za Maswahaba uzushi wa Qaadiriyyah ukajitokeza. Msingi wa Bid’ah zao ulitokana na udhaifu fahamu zao kuhusu kuyafahamu mahitaji ya kuwa na Imaan kuhusu Qadar ya Allaah na Imaan katika amri za Allaah na makatazo Yake ... Na ma-Khawaarij wakazungumzia kuhusu kuwakufurisha wenye kufanya madhambi miongoni mwa wenye kuelekea Qiblah wanaposema: “Kwa hakika wao ni makafiri watakaokuwa Motoni milele”. Watu wakajiingiza kwenye mijadala hii, na ma-Qaadiriyyah wakajishughulisha na haya baada ya kifo cha al-Hasan al-Basree.

(Endelea Kutoka Uk. 2)

'Amroo' Bin 'Ubayd na wenzake walisem,a: "Wao si Waislamu wala si Makafiri, bali wao wako mahali baina ya sehemu mbili na watakuwa Motoni milele na kwamba hawana chochote katika Uislamu wala Imaan, ingawaje hawakuwaita wao kuwa ni makafiri."
Kwa njia hii, ugonjwa wa takfeer bila ya dalili ya kisheriya iliyo wazi, ukaanza kufifia kutoka kwenye pote moja la Ahlul-Bid'ah hadi jengine mpaka ikawa ndio alama yao yenye kuwatambulisha na alama ya wazi ya pote la kawaida la watu wa Bid'ah.
Abdul-Qahir al-Baghdadi amesema: "Hakuna pote kutoka katika mapote ya upinzani, isipokuwa wanawakufurisha wenzao, mmoja kwa mwengine, nao wanajitakasa mmoja kutoka kwa mwengine, kama ma-Khawaarij, Rawaafidh na ma-Qadariyyah, kiasi cha kwamba hukutana kwenye mikutano na kuacha kukufurishana wao kwa wao."
Amesema Sheykhul Islam Ibn Taymiyyah (رحمه الله): "Wengi miongoni mwa Ahlul-Bid'ah, kama vile ma-Khawaarij, Rawaafidh, Qadariyyah, Jahmiyyah na Mumath-Thilah walikuja kukatikiwa kushikamana na Imani ya Upotofu , lakini wao wakaionelea kuwa ni Haki na wakawachukulia wenye kuwapinga wao katika hilo kuwa ni Makafiri." Vilevile akasema: "Miongoni mwa hali za Ahlul-Bid'ah ni kwamba wao huzua matamshi au maneno. Wao huitakidi maneno hayo kuwa ni Uwajibikaji katika Dini, bali huyafanya kuwa ni katika sehemu ya Imaan ambayo ni waajib juu ya kila mtu. Wao humkufurisha kila mwenye kuwapinga kwa hilo na kuhalalisha damu zao, kama wafanyavyo ma-Khawaarij, Rawaafidh, Jahmiyyah na Mu'tazilah na wengineo. Ahlus-Sunnah hawazui misemo, wala hawawakufurishi wenye kufanya makosa baada ya kufanya Ijtihaad, hata kama wanawapinga, na kuwakufurisha Ahlus-Sunnah, wakazihalalisha damu zao. Kama ambavyo Maswahaba hawakuwakufurisha ma-Khawaarij, hata kama walimkufurisha 'Uthmaan na 'Alee na waliowaunga wao mkono, na hata kama walizihalalisha damu za Waislamu."
Ibn Abul-Izz al-Hanafee (رحمه الله) amesema: "Miongoni mwa sura za aibu za Ahlul-Bid'ah ni kule kukufurishana wao kwa wao. Na miongoni mwa sura za kusifika za watu wenye 'ilmu ni kwamba wao husema fulani Bin fulani amefanya makosa na hawamkufurishi."

YANYOHUSIANA NA RIWAYA YA UZUSHI KATIKA KITAAB AT-TAWHEED

NA: SHEIKH MUHAMMAD BIN SAALEH AL-'UTHAYMEEN (رحمه الله)

Yakwamba Ibn 'Abbaas amesema: "Ama kuhusu aya isemayo: **"Basi anapowapa (mtoto) mwema (kamili) wanamfanyia washirika Allaah katika kile alichowapa (Naye ni yule mtoto). Ametukuka Allaah na huko kushirikisha kwao."** [al-A'raaf 7:190]. Pindi Adam (عليه السلام) alipojumuika pamoja na Hawaa', alishika mimba, kisha Iblees akamjia na akamwambia: "Mimi ni rafiki yako niliyekusababisha ukafukuzwa kutoka Peponi. Sasa nitwi'i mimi, au nitanfanya mtoto wako amee pembe mbili kama Paa, ambazo atakazokukutoboa nazo tumbo lako atakapotoka! Kwahivyo, fanya hivyo! Kwahiyo akajaribu kuwatisha wamwite mtoto wao abul-Haarith, lakini hawakumtwi'i kwa hilo, mara wakamzaa mtoto aliyekufa. Mara ya pili Hawaa' aliposhika mimba, Iblees akawajia tena na akarudia madai kama ya kwanza, lakini wakamkatalia tena na akazaliwa tena mtoto aliyekufa. (Hawaa') akashika mimba mara ya tatu na Iblees akawajia tena na kuwakariria madai kama yale ya kwanza, akiwakumbusha kuhusu yaliyotokea hapo awali. Hapo ndipo walipozidiwa na mapenzi (mahaba) ya mtoto wao (waliyemtarajia) ikawabidi wamuite kwa jina hilo la Abul-Haarith, na hii ndiyo sababu ya Allaah (سبحانه وتعالى) akasema: **"wanamfanyia washirika Allaah katika kile alichowapa."** [al-A'raaf 7:190].
Sheikh Ibn 'Uthaymeen amesema: "Na kisa hiki ni cha urongo kutokana na njia nyingi."

1. Yakwamba hakuna riwaya iliyo swaheeh kuhusiana na kisa hicho kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم), na ni miongoni mwa sampuli za visa visivyoweza kupatikana isipokuwa kwa njia ya Wahyi, na akasema Ibn Hazm kuhusiana na kisa hiki, "Kwa hakika ni kisa cha urongo wa ushirikina."
2. Lau kama kisa hiki kilikuwa ni cha kuwahusu Adam na Hawaa', basi emma waliwahi kutubia kutokamana na shirk au walikufa nayo, kwahiyo yoyote mwenye kuruhusu kukubali yakwamba mmojawapo miongoni mwa Mitume alikufa juu ya Shirk, basi hilo ni jambo lililo baya sana. Na kama walitubia kutokamana na shirk, basi hilo halifaidishi chochote katika hikma, uadilifu na Rehma za Allaah, yakwamba Ameyataja makosa yao na wala sio toba yao kutokana na makosa hayo. Pindi Allaah (سبحانه وتعالى) anapotaja makosa ya baadhi ya Mitume yake na Manabii, hutaja toba zao kutokamana na makosa yenyewe, kama ilivyo kwenye kisa cha Adam na Mkewe, Hawaa', alipokula kutoka kwenye Mti na wakatubia kutokamana na makosa hayo.
3. Yakwamba Mitume wamehifadhiwa kutokamana na shirk kwa maafikiano ya wanavyuoni.
4. Yakwamba imethibitishwa kwenye hadeeth ya Shifaa', yakwamba watu watakuja kwa Adam watafute shifaa' kutoka kwake, basi atajiombea nafsi yake, kutokana na kosa la kula kutoka kwenye Mti huo na hayo yalikuwa ni makosa, na lau kama shirk imetokana nae, basi ingelikuwa ni msamaha mkubwa.
5. Yakwamba kwenye kisa hiki imetajwa kuwa Sheitwaan aliwajia akawaambia: "Mimi ndiye rafiki yenu niliyewatoa Peponi", kwahivyo ikiwa alisema hivyo, basi wangelijua kwa yakini yakwamba alikuwa ni adui kwao na wala hangelikubali chochote kutoka kwao.
6. Yakwamba kwenye kisa hiki palikuwa na maneno yake: "Nitaisababisha iwe na pembe zitakazotoboa tumbo lako ...". Lau kama angeliamini yakwamba kwa hakika pangelikuwa na uwezekano wa kufanya hivyo , basi hiyo ingelikuwa ni shirk katika Uola kwa sababu hapana awezae kufanya hivyo . Na lau kama hakuamini yakuwa ilikuwa yawezekana, basi

(Endelea kwenye Uk. 4)

haiwezekani kwake kuamini maneno yake.

7. Maneno ya Allaah (سبحانه وتعالى): **"Ametukuka Allaah na huko kushirikisha kwao."** [al-A'raaf 7:190].

Hapa kiwakilishi nomino ni kwa wingi na lau kama ilikuwa inamuhusu Adam na Hawaa', basi ingelitamkwa kwa njia ya wawili ... Lakini lililo la sawa ni alilosema al-Hasan (رحمه الله): "Kwa hakika waliokusudiwa katika aya hii sio Adama na Hawaa'." na lililokusudiwa ni washirikina miongoni mwa watoto wa Adam (wanawe), kama ilivyobainishwa na Ibn Katheer katika Tafseer yake. Tizama katika al-Qawl al-Mufeed 2/156-157.

UMUHIMU WA KUREKEBISHA MAKOSA BADALA YA KUYANYAMAZIA

Mtu mjinga anahitaji kufundishwa; na mwenye shaka anahitaji kuwekewa mas'ala waziwazi; na mwenye kughafilika anahitaji kukumbushwa; na mwenye kufanya makosa kwa kukusudia anahitaji kuonywa. Si jambo la sawa kumchukulia mwenye kujua kuhusiana na mas'ala fulani na asiyejua kuhusiana na mas'ala hayo kwenye upeo mmoja unapowalaumu. Kumkaripia asiyejua kwa ukali hakuto ongeza isipokuwa ni kumkimbiza na kumfanya akatae naswiha zako, kinyume cha kumfundisha kwa hikma na upole, kwa sababu mtu mjinga huwa haonu yeye kuwa anafanya makosa. Ni kama kwamba anamwambia Yule mwenye kumkaripia: "Basi kwanini kwanza hunifundishi kabla ya kunishambulia?"

Mwenye kufanya makosa bila ya kukusudia, huwenda akadhania yakwamba yeye yuko kwenye usawa, kwahivyo inatupasa kuyazingatia hayo ili tupate muelekeo mzuri wa maendeleo. Amepokea Imaam Ahmad (رحمه الله) katika Musnad yake kutoka kwa al-Mugheera Ibn Shu'bah: "Mtume (صلي الله عليه وسلم) alikula chakula, kisha akasimama na kuanza kuswali. Alikuwa tayari ameshatawadha kabla ya hapo, lakini mimi nilimletea maji ili apate kutawadha. Akanipuuza kisha akaniambia, "Nenda zako!" Nikaona vibaya, Wallaahi". Akaswali kisha akenda kwa 'Umar na kumlalamikia kuhusu hayo yaliyotokea. 'Umar akenda kwa Mtume (صلي الله عليه وسلم) akamwambia: "Yaa Rasoolullaah, al-Mugheera ameona vibaya kwa jinsi ulivyompuuza, na ana wasiwasi pengine huwenda ikawa umemkasirikia kwa sababu fulani." Mtume (صلي الله عليه وسلم) akamwambia: "Mimi namuona kuwa ni mtu mzuri, lakini amenileta maji ili nitawadhie baada ya kula chakula. Na lau kama ningelitawadha, basi watu wangelichukuwa hayo kuwa ndiyo mafunzo yangu (wangelidhani kuwa kila wamalizapo kula itawabidi watawadhe) [*al-Musnad*, 4/253].

Hapa inatupasa kuzingatia yakwamba, wakati Mtume (صلي الله عليه وسلم) alipotaja makosa ya Swahaba huyu Mtukufu, haikuwa na sura mbaya kwake au hakumkata na kuachana nae, palikuwa na hikma ya busara. Na lau kama hangelipata fursa hii ya kukosolewa na Mtume (صلي الله عليه وسلم), angelikuwa kwenye hali ya wasiwasi mkubwa, akawa anajituhumu nafsi yake, mapaka awe na hakika yakwamba Mtume (صلي الله عليه وسلم) alikuwa radhi nae.

INGIA KWENYE UISLAMU KWA UKAMILIFU

NA: SHEIKH MUHAMMAD AL-JIBAALY

(Endelea Kutoka Vol. 100, Issue 5)

MTUME (صلي الله عليه وسلم) KUHUSU "GANDA" (LA TUNDA)

Kama tulivyo-onyesha hapo awali kuwa Mtume (صلي الله عليه وسلم), Maswahaba zake (رضي الله عنهم), na Salaf wema katika zama zote wameubeba Uislamu kwa ukamilifu. Mtume (صلي الله عليه وسلم) hakuona tafauti baina ya kunyo-osha Swafu katika swala na kuongoza jeshi katika ushindi, wala baina ya kuamrisha watu kukuuza ndevu zao na kuweka msingi wa Taifa lililo na nguvu kuliko Mataifa yote katika historia. Jambo la kushangaza lenye kutiliwa nguvu zaidi ni kule kuwa Mtume (صلي الله عليه وسلم) alifanya hilo linaloitwa ganda kuwa ni alama ya kilichofichwa katika tabia. Ganda lenye swiha nzuri na lenye kunawiri basi kwa kawaida huwa na ndani ya lile tunda pia ni lenye swiha na uzuri. Ama ganda lililo sinyaa au kunywea linalo onyesha magonjwa basi kwa kawaida na ndani ya tunda huwa mambo si mazuri.

An-Nu'maan Bin Basheer (رضي الله عنه) alipokea kuwa Mtume (صلي الله عليه وسلم) alikuwa akiwanyoosha Maswahaba zake katika swafu za swala kama mshale ulionyooka, na akasema: "Waja wa Allaah mtazifanya sawa kwa kuzinyoosha swafu zenu au Allaah atazifanya nyuso zenu kutafautiana." [Muslim, Aboo Dawood na wengineo].

Kwenye hadeeth nyengine alisema: "Nyosheni swafu zenu au Allaah atazifanya nyoyo zenu kukhitalifiana". [Aboo Daawud na Ibn Hibbaan- aliiswahihisha al-Albanee – swaheeh ut-Targheeb wa Tarhib vol. 1 Uk.275)

Hili wazi laonyesha kuwa kutoafikiana kwa Waislamu hata katika mambo "madogo" kama kunyoosha swafu, huleta kuchukiana kukubwa kwa nyoyo zao na ikhlitaaf baina yao.

Mtume (صلي الله عليه وسلم) alikuwa na hamu kubwa ya kuwataka Maswahaba zake waonyeshe umoja, hata katika kikao. Jabir bin Samurah (رضي الله عنه) alihadithia kuwa siku moja Mtume (صلي الله عليه وسلم) aliingia msikitini na akawaona Maswahaba zake wamekaa vikundi vikundi. Akawakemea kwa kusema: "Mbona nawaona nyinyi mmegawanyika (katika makundi)?

Vile vile Abu Tha'alabah al-Khushani (رضي الله عنه) alihadithia kuwa walipokuwa wakisimama kwa ajili ya kupumzika wakiwa safarini na Mtume (صلي الله عليه وسلم), watu walikuwa wakitawanyika miongoni mwa vilima na mabonde, kwahiyo Mtume (صلي الله عليه وسلم) akasema: "Hakika kutawanyika kwenu katika vilima na mabonde hayo hakika yatoka kwa sheitani" walivyokuwa (Maswahaba) wepesi wa kuchukuwa mafunzo walikuwa kuanzia siku hiyo wakikaa pamoja kwa ukaribu kiasi cha kwamba lau utachukua nguo moja waweza kuwafunika wote. [Aboo Dawood Ibn Hibban na wengine- imeswahihishwa na al-Albaani – jilbaab al-mar'at al-muslimah Uk.211].

MWISHO

Njia iliyo swaheeh kuupata Uongofu na mafanikio ni kwetu sisi kuswahihisha matendo yetu ya wazi kwa kushikamana na Sunnah kwa ukamilifu, na nyoyo zetu kwa ikhlaas na kuendelea kuwa waangalifu juu ya mambo ya Allaah (سبحانه وتعالى). Twamuomba atupe taufiq katika kuupata uongofu na kuipenda Sunnah ya Mtume Wake (صلي الله عليه وسلم).